**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KUPOKEA TAARIFA YA TIMU YA TATHMINI KILICHOKAA KATIKA OFISI ZA MANUNUZI TAREHE 29/11/2021**

**MAHUDHURIO:**

1. Peres Kamugisha - Mwenyekiti
2. Samson Manjale - Katibu
3. Simon Sambalu - Mjumbe
4. Amos Kanige - Mjumbe
5. Venance Hanje - Mwanasheria

**WAALIKWA:**

1. Hassan Kinonono - Mhandisi
2. Amon Ngonyani - Fundi sanifuUjenzi
4. Irene Mville - CBCTC – Likuyusekamaganga
5. Robert Makenge - CBCTC – LikuyuSekamaganga
6. Joseph Mtoi - CBCTC - LikuyuSekamaganga

**SEKRETARIETI:**

1. SiwetuPilly - Sekretarieti

**AGENDA ZA KIKAO:**

**1. AGENDA Na CBCTC/NMT/2021/2022/1: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 10:40 Asubuhi aliwaomba wajumbe waweze kuchangia mada kwa umakini nakupitia Taarifai iyowasilishwa kwa kuangalia sifa na uwezo wa waombaji.

**2. AGENDA Na. CBCTC/NMT/2021/2022/02 KUJADILI TATHMINI YA BEI ZA MAFUNDI**

Mwenyekiti alimkaribisha Katibu aweze kusoma Taarifa ya Timu ya Tathimini kama ilivyoandaliwa na kuwasilishwa kwa Bodi ya Zabuni. Katibu alisoma kwa mchanganuo ufuatao:-

**A: UKARABATI WA JENGO LA OFISI(CBCTC/NMT/2021/2022/W/01/Lot 1)**

Kazi hii iliombwa na mwombaji mmoja YustinaKambanga, kwabeiyaTshs. 22,940,000/=.Timu ya Tathimini ilipitia nyaraka zilizowasilishwa na mwombaji na kuona kuwa zipo sahihi na amekidhi vigezo vilivyowekwa.

Timu ya tathimini ilipendekeza kuwa kazi hii ifanywe naYustina Kambanga kwa gharama ya shilingi 22,940,000.00 LAKINI aitwe kwenye majadiliano kwakuwa bei yake imevuka kiwango cha makisio ya Mhandisi ambayoni Tshs. 7,300,000.00.

**MAAMUZI YA BODI**

Baada ya kujadiliana bodi ya zabuni ilimpitisha Yustina Kambanga afanye kazi hii kwa gharama ya shilingi 22,940,000.00 lakin iagizo la timu ya tahimini litekelezwe kasha taarifa ya majadilaino iwasilishwe Bodi ya zabuni.

**B: UKARABATI NYUMBA MBILI (2) ZA WATUMISHI (CBCTC/NMT/2021/2022/W/01LOT 2**

Kazi hii iliombwa na waombaji wawili Ndomba Edson aliombakwaTShs. 17,250,000/= na Hamisi Mwanzagi aliomba kwaTshs. 17,573,135/=

Lakini Edson Ndomba alitolewa kwa kuwa aliomba kazi mbili kinyume na tangazo lilivyotaka.

Timu ya Tahimini ilipitia nyaraka za Hamisi Mwanzagi na kuona kuwa zipo sahihi na amekidhi vigezo vilivyotolewa.

Hivyo timu ya tathimini ilipendekeza kazi hii apewe Hamisi Mwanzagi kwa gharama ya shilingi 17,573,135/= lakini aitwe kwenye majadiliano kwa kuwa kiasi alichotaja kimezidi makisio ya Mhandisi ambayo ni Tshs. 16,341,030.

**MAAAMUZI YA BODI**

Baada ya majadiliano Bodi ya Zabuni ilimpitisha Hamisi Mwanzagia fanye kazi hii kwa gharama ya shilingi 17,573,135.00 lakini aitwe kwenye majadiliano.

**C: UKARABATI WA BWENI NA UJENZI WA UZIO (CBCTC/NMT/2021/2022/W/01/LOT 3)**

Kazi hii iliombwa na waombaji wawili ambao niNdomba Edson aliombakwaTshs. 7,220,000/=na Venant P.Mponda aliomba kwa Tshs. 38,880,000/=.

Timu ya tathimini ilipitia nyaraka zilizowasilishwa na Venant Mponda na kuona kuwa zipo sahihi na kupendekeza afanyekazi hii.

Timu ya tathimini ilipendekeza kuwa kazi hii apewe Venant Mponda kwa gharama ya shilingi 38,880,000.00 lakini aitwe kwenye majadiliano kwa kuwa bei aliyoombea tajaimezidimakisioyaMhandisi.

**MAAMUZI YA BODI**

BodiyaZabuniilipitishakazihiiapeweVenantMpondakwagharamayaTshs. 38,880,000.00 Lakiniaitwekwenyemajadilianokamatimuyatathiminiilivyoshauri.

**3. AGENDA Na CBCTC/NMT/2021/2022/3. UJENZI WA MATUNDU YA VYOO:**

Kazi hii iliombwa na mwombaji mmoja Mohamed Rabana LupiakwaTshs. 8,002,000/=.

Timu ya tathimini ilipitia nyaraka zote na kuona kuwa zipo sahihi na anazo sifa kama zilivyoaiinishwa kwenye tangazo.TimuyaTahimin iilimpitisha Mohamed Rabana afanye kazi hii lakini aitwe kwenye majadiliano kwa kuwa maombi yake yamevuka makisio ya mhandisi.

**MAAMUZI YA BODI**

Wajumbe kwa Pamoja walipitisha kuwa kazi hii ifanywe na Mohamed Rabana Rupia kwa gharama ya Tshs. 8,002,000 lakini aitwe kwenye majadiliano.

**4.AGENDA Na.. AGENDA Na CBCTC/NMT/2021/2022/4 IDHINI YA KUTUMIA "FORCE ACCOUNT" KATIKA UJENZI WA MADARASA YA UVICO 19**

Mwenyekiti alimpa Nafasi Katibu wa kikao, ambaye aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri imepoke fedha Tsh. Bilioni Moja Nukta sita (Tsh. 1,600,000,000.00) kwa ajili ya madarasa ya shule za sekondari na kiasi cha Tsh. Milioni Mia moja Ishirini (Tsh. 120,000,000.00) kwa ajili ya

madarasa ya shule za msingi.kwa ajili ya Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa madarasa ya UVICO 19. Baada ya taarifa hiyo fupi Katibu aliwasilisha maombi ya kutumia "Force Account" katika kutekeleza mradi huo.

**MAAMUZI YA BODI**
Wajumbe kwa Pamoja waliridhiaa maombi yaliyowasilishwa kwamba ujenzi wa madarasa utatekelezwa kwa kutumia 'Force Account"

**5. AGENDA Na. CBCTC/NMT/2021/2022/W/01/:3 KUFUNGA KIKAO:**
Mwenyekitialiendeleakuwasisitizawajumbekuwasimamiamafundikwakaribu Zaidi iliwaweze Kumalizakazikwamudamuafakana fundi asiyekuwanamafundiwakutosha au asipoonekana site Basimkataba wake uvunjwe mara mojanakupewa fundi mwingine. Mwenyekitialiwashukuru Wajumbekwamichangoyaonaalifungakikaomnamo Saa 11:52 Asubuhi.

*UMETHIBITISHWA*

…………………
MWENYEKITI

………………………
KATIBU

TAREHE 30/11/2021